**Richmond County School System (Mfumo wa Shule wa Kaunti ya Richmond)**

**Taarifa ya Mzazi kuhusu Ustahiki na Uwekaji wa Kwanza wa Mwanafunzi wa Kiingereza (EL) katika Mpango wa Kiingereza kwa Wazungumzaji wa Lugha Zingine (ESOL) na Huduma za Nyongeza za Mafundisho ya Lugha za Title III**

**Jina la Mwanafunzi**: ____________________ **Tarehe**: ____________

**Shule:** ____________________ **Gredi:** ____________

Mpendwa Mzazi/Mlezi:

Tunataka kukuarifu kwamba mwanafunzi wako anatimiza vigezo vya ustahiki kwa mwanafunzi wa Kiingereza na anastahiki kupata huduma za mpango wa lugha wa ESOL.

Kulingana na majibu yako ya maswali ya Utafiti wa Lugha ya Nyumbani wakati wa usajili, shule ilichunguza kiwango wa mwanafunzi wako cha ustadi wa lugha ya Kiingereza. Alama ya mwanafunzi wako (angalia hapa chini) zinaonyesha kwamba atanufaika na huduma za mafundisho ya lugha ili kukuza ustadi wa Kiingereza. Lengo letu ni kumsaidia mwanafunzi wako kukuza ustadi wa Kiingereza cha kimasomo unaohitajika ili kufaulu shuleni.

| | Jina la Mtihani na Viwango vya Gredi | Tarehe ya Mtihani | Kiwango cha Mwanafunzi wako cha Ujuzi wa Lugha ya Kiingereza | Alama za Kiwango cha Ustadi Zinazofanya Astahiki |
|---|---|---|---|---|
| ☐ | **WIDA Screener (K)** kwa muhula wa 1 Chekechea | | Alama za Jumla za Lugha ya Kunena ____________ | Alama za Jumla za Lugha ya Kunena 1.0-4.9 |
| ☐ | **WIDA Screener (K)** kwa Muhula wa 2 na Muhula wa 1 Gredi ya 1 | | Mchanganyiko wa Jumla: ________ | Mchanganyiko wa Jumla 1.0-4.9 |
| ☐ | **WIDA Screener (1-12)** kwa Muhula wa 2 Gredi ya 1 | | Mchanganyiko wa Jumla: ________ | Mchanganyiko wa Jumla 1.0-4.9 |
| ☐ | **WIDA Alternate Screener (K-12)** | | Mchanganyiko wa Jumla: ________ | Mchanganyiko wa Jumla 1.0-4.9 |
| ☐ | Chini ya vikoa vinne vya lugha:<br>☐ **WIDA Screener (K-12)**<br>☐ **Alternate Screener (K-12)** | | Kiwango cha ELP cha mtoto wako: _ | Vikoa Vyovyote Vilivyotahiniwa 1.0-4.9 |
| ☐ | **Mtihani wa Ustahiki wa Nje ya Jimbo**<br>____________ | | Alama ya Ustahiki: ____________ | Jimbo: ____________ |

Mwanafunzi wako hupokea mafundisho ya lugha kupitia Mpango wetu wa Lugha wa ESOL wa shule. Mpango huu huwasaidia wanafunzi kukuza ujuzi muhimu wa Kiingereza katika kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika, ili kusaidia kufikia matarajio ya kiwango cha gredi. Walimu wetu wa ESOL wanasaidia ujifunzaji wa wanafunzi na kufuatilia maendeleo yao katika Kiingereza.

Mwanafunzi wako anapokea huduma za Mpango wa Lugha wa ESOL kupitia muundo wa mafundisho uliobainishwa kwenye upande wa kushoto kwenye chati hapo chini. Aidha,

☐ Mtoto wako pia anapokea huduma za nyongeza za mafundisho ya lugha ili kukuza ujuzi wa lugha ya Kiingereza na kusaidia mafanikio ya kimasomo. Angalia upande wa kulia kwenye chati iliyo hapa chini.

☐ Mtoto wako hapokei huduma za nyongeza za mafundisho ya lugha.

**Richmond County School System (Mfumo wa Shule wa Kaunti ya Richmond)**

| Muundo wa Mafundisho ya Mpango wa Lugha wa ESOL | Huduma za Nyongeza za Mafundisho ya Lugha za Mpango wa Title III |
|---|---|
| ☐ **Kuondolewa**: Mwanafunzi wako anaondoka darasani wakati wa ______________________ ili kujifunza Kiingereza katika kundi ndogo pamoja na mwalimu mtaalamu wa ESOL.<br>☐ **Kujumuishwa**: Mwanafunzi wako anabaki darasani wakati mwalimu mtaalamu wa ESOL anapotoa msaada wa ziada wa lugha wakati wa ________________.<br>☐ **Darasa Lililoratibiwa la ESOL:** Mwanafunzi wako anaenda darasa pamoja na wanafunzi wengine wa Kiingereza, ili kujifunza Kiingereza cha kijamii na lugha ya kimasomo ya masomo ya shule. | Mtoto wako anapokea huduma za mafunzo ya lugha ya ziada za Title III:<br>☐ **Lexia Core5**: Mpango wa ziada wa mafunzo ya kibinafsi mtandaoni ambayo husaidia wanafunzi wa Kiingereza katika chekechea hadi gredi ya 5 kuongeza ustadi wa Kiingereza.<br>☐ **Flashlight 360**: Mpango wa nyongeza wa mtandaoni unaowasaidia wanafunzi wa Kiingereza katika gredi za 1-5 kuboresha ujuzi wa kuzungumza na kuandika.<br>☐ **Summit K-12**: Mpango wa ziada wa mafunzo ya kibinafsi mtandaoni ambayo husaidia wanafunzi wa Kiingereza katika gredi ya 6-12 kuongeza ustadi wa Kiingereza. |

Unaweza kuangalia maendeleo ya kimasomo ya mwanafunzi wako kwa kuingia kwenye Infinite Campus katika https://campus.rcss-k12.org/campus/portal/richmond.jsp.

Ikiwa mwanafunzi wako yuko katika shule ya upili, kiwango cha kuhitimu kwa wanafunzi wa Kiingereza katika 2023-2024 kilikuwa 72%.

Baada ya mwanafunzi wako kufikia kiwango kinachohitajika cha ujuzi wa Kiingereza kwenye mtihani wa *WIDA ACCESS* au *Alternate ACCESS*, mwanafunzi wako hataainishwa tena kama mwanafunzi wa Kiingereza anayehitaji usaidizi wa mpango wa lugha wa ESOL.

Iwapo mwanafunzi wako ana ulemavu, wafanyakazi wetu wa usaidizi wa elimu maalum na lugha wataeleza jinsi huduma za lugha ya Kiingereza zinavyojumuishwa katika Mpango wa Elimu Binafsi (IEP) wa mwanafunzi wako. Walimu wa ESOL hushirikiana na mwalimu wa elimu maalum ili kumpa mwanafunzi wako huduma za usaidizi za lugha zilizoelezwa katika IEP.

Una haki ya kukataa huduma za mpango wa lugha wa ESOL kwa mwanafunzi wako. Ikiwa ungependa kuondoa huduma hizi, kujadili chaguo zingine za mpango, au kupata maelezo zaidi kuhusu mikutano yetu ya wazazi, tafadhali wasiliana na mtu aliyetajwa hapa chini.

Tuko hapa kukusaidia wewe na mwanafunzi wako. Tafadhali wasiliana nasi ikiwa una maswali yoyote au ungependa kujadili hili zaidi na wafanyakazi wetu katika lugha unayopendelea. Asante.

Asante

**Jina:** ________________________________________ **Cheo:** ______________________________

**Namba ya Simu:** ________________________________ **Barua pepe:** __________________________